# Uchimuzi wa Fikra za Kijaala katika Ushairi wa Kiswahili: Mifano Kutoka *Tungizi za Mnyagatwa* na *Diwani ya Midulu*

Hassan R. Hassan
Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro

Athumani S. Ponera
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere
atponeraman@gmail.com

**MAKALA HALISI**

**HISTORIA YA MAKALA**

***Kupokelewa:****05 Machi 2022*

***Kurekebishwa:****15 Juni 2022*

***Kukubaliwa:*** *29 Julai 2022*

***Kuchapishwa:*** *20 Septemba 2022*

**ISSN: 2799 – 2187**

*Juzuu 1, Toleo 1, uk. 17 – 33.*

**NUKUU**

Hassan, H. R. & Ponera, A. S. (2022). Uchimuzi wa Fikra za Kijaala katika Ushairi wa Kiswahili: Mifano kutoka Tungizi za Mnyagatwa na Diwani ya Midulu. *Jarida la Fahari ya Kiswahili, 1*(1), 17 – 33.

**Ikisiri**

Makala hii imechunguza fikra za kijaala zinazosawiriwa katika ushairi wa Kiswahili. Makala imetokana na utafiti wa kimaktaba. Data zilipatikana kwa njia ya usomaji na uchambuzi wa matini mbalimbali na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya usimbishaji wa maudhui. Matokeo yamewasilishwa na kujadiliwa kwa kutumia nadharia ya Ujaala. Matokeo yanaonesha kuwa diwani teule zilizochunguzwa zimesawiri fikra za kijaala kupitia mianzo na miisho ya mashairi, falsafa kuhusu uwezo wa kutunga mashairi na mielekeo ya vipengele vya kimaudhui vinavyohusu uhai, ndoa, uzazi, ibada na kifo. Makala hii inapendekeza kufanyika kwa uchunguzi zaidi kuhusu uwezo na kiasi cha tanzu nyingine za fasihi ya Kiswahili kusawiri ujaala. Pia, uchunguzi unaweza kufanyika ili kulinganisha uwezo na kiasi cha usawiri wa ujaala kati ya fasihi na tawi lingine lolote la sanaa au baina ya fasihi ya jamii ya Waswahili na ya nje ya jamii ya Waswahili.

**Istilahi za Msingi**: Uchimuzi, ujaala, ushairi, fikra, falsafa na itikadi.

## 1.0 Utangulizi

Makala hii inafafanua fikra anuwai za kijaala zinazosawiriwa katika diwani teule za ushairi wa Kiswahili. Ujaala unahusiana na nguvu au kani maalumu inayotawala kuwapo kwa ulimwengu, walimwengu na mambo mbalimbali yanayowahusu. Kani hii iko bayana kwa kila kiumbe razini aliyepo

ulimwenguni. Kietimolojia, neno jaala limetokana na maneno mawili, ambayo ni 'mja' na '*Allah*' (Ponera, 2014). 'Mja' maana yake kiumbe, *Allah* ni neno la Kiarabu linalomaanisha Mungu. Maneno yote haya mawili yananasibishwa na dini ya Uislamu. Hata hivyo, pamoja na istilahi ya ujaala kuchipuka kutoka kwenye muktadha wa dini ya Uislamu, ukweli ni kwamba, kimatumizi, dhana ya ujaala haifungwi tu katika mawanda ya dini hiyo pekee.

Ujaala huweza kuelezwa kwa mielekeo mikubwa miwili, ki-dhana na ki-nadharia (Hassan, 2018). Mwelekeo wa ki-dhana huuelezea ujaala kwa kuegemea katika dhana za falsafa na itikadi. Ujaala kama dhana ya kifalsafa hurejelea undani wa mfumo wa fikra ambao mtu au jamii huuegemea katika kuendesha maisha yao. Ujaala kama dhana ya kiitikadi humaanisha nyenzo ambayo mtu au jamii huitumia kufikia kilele cha mfumo anaouegemea (Ponera, 2019). Mwelekeo wa ki-nadharia huuelezea ujaala kama umbo kuu lenye kubeba dhana mbalimbali, pamoja na uelekeo wa kifikra unaotokana na mkusanyiko wa misingi husika.

Dhana ya ujaala ilikuwepo hata kabla ya kuzaliwa kwa Kristo. Mathalani, fikra hizi zinaonekana kupitia wanafalsafa wa mwanzo wa Kiyunani kama vile Sokrates Sophroniscus, Aristocles Ariston Plato na Aristotle Nicomachus (Senkoro, 1987 &Ponera, 2010). Katika uga wa fasihi, mawazo ya kijaala yanaanza kujitokeza kwenye nadharia zinazoelezea chimbuko la fasihi. Mojawapo ya nadharia hizo inaeleza kuwa chimbuko la fasihi ni Mungu. Wafuasi wa nadharia hii wanaamini kuwa Mungu ndiye msanii mkuu aliyeuumba ulimwengu kwa usanii wa ajabu. Nadharia hiyo inamwona mwanadamu kama zao la Mungu. Pia, inaamini kuwa chimbuko la sanaa ni jazba inayompata msanii. Mawazo haya yanafungamana na dhana ya ujaala ambayo inaamini kuwa kila jambo linalomfika binadamu hukadiriwa na Muumba wake mwenye uwezo wa kuyaendesha maisha yake.

Mawazo haya ya kijaala yaliendelea kuwaathiri wasomi wa mwanzo wa Kiyunani, hasa Hesiod na Plato (Mulokozi, 2017). Katika fasihi na maisha ya Waswahili, mawazo haya yameendelea kujitokeza kupitia fikra za wataalamu kama vile Nkwera (1976). Mlaga (2017) anabainisha kuwa mawazo ya namna hii yanajitokeza hata sasa katika jamii ya Wasukuma nchini Tanzania ambapo manju huaminika kupata uwezo wa kuimba kutokana na kuchanjiwa dawa za

asili. Wamitila (2003) anadai kuwa ujaala ni mtazamo wenye misingi ya kidini. Izingatiwe kuwa, dhana ya dini hapa inatumika kurejelea imani yoyote ambayo kiumbe razini wa ulimwengu huu huifuata au huwa nayo kuhusu kani inayoongoza mustakabali wa kuwapo kwake. Akishadidia hoja hii, Hameed (2011) anasema:

> Waislamu ulimwenguni kote huishi katika wingu la ujaala na kutokuwa na hakika kuhusu yatakayowatokea katika nyakati zijazo. Wakati Kurani pia imeweka msisitizo katika uhuru wa maamuzi pamoja na mienendo ya kimaadili ya mtu binafsi na kijamii, fikra na matendo yao kwa kawaida ni ya kijaala sana (uk. 21).

Ingawa imani kuhusiana na ujaala ina misingi ya kidini, lakini huwa na tofauti katika kuiendea kati ya jamii moja na nyingine. Tofauti hii hutokana na kila jamii kuwa na itikadi yake. Tofauti hiyo haiwi kwa ngazi ya jamii tu, bali hata baina ya mtu na mtu. Mathalani, kuna baadhi ya jamii huamini kuhusu uwepo wa Mungu na nyingine huamini kuhusu miungu, mizimu na vitu vingine kama vile miti, mapango, hirizi na majabali. Imani zote hizo huwaelekeza katika kuitakidi kuwa kuna kani inayowaongoza katika maisha yao. Kani hiyo huwa mtu hawezi kushindana wala kupingana nayo.

Jamii za Wayunani zilikuwa zikiamini katika Mungu na miungu mbalimbali iliyokuwa ikiwasaidia katika mambo yao. Cuddon (1998) anabainisha kuwa *Muse* ni jina lililorejelea Mungu yeyote kati ya miungu tisa ya Wayunani ambayo ni watoto wa *Zeus* na *Mnesmosyne*. Miungu hiyo ilikuwa na mgawanyo katika kutawala aina mbalimbali za sanaa. Katika mgawanyo huo, kuna *Calliope* (Mungu wa ushairi na tendi), *Clio* (Mungu wa historia), *Urania* (Mungu wa unajimu) na *Erato* (Mungu wa ushairi wa mapenzi). Pia, kuna *Euterpe* (Mungu wa ushairi wa tumbuizo), *Melpomene* (Mungu wa tanzia), *Polyhmnia* (Mungu wa ushairi wa kusifu Miungu), *Terspsichone* (Mungu wa dansi) na *Tnalia* (Mungu wa ufutuhi).

Ponera (2014) anaitaja miungu mingine iliyoaminiwa na jamii ya Wayunani na Warumi kuwa ni *Saturnalia* (Mungu wa mazao au mavuno), *Cupid* (Mungu wa mapenzi), *Aesculapius* (Mungu wa dawa), *Minerva* (Mungu wa uwindaji) na *Samnus* (Mungu wa usingizi). Kwa ujumla, miungu hawa walihusishwa na

matukio yaliyokuwa yanawatokea wanajamii. Pia, Wayunani walikuwa wakiamini katika utabiri kuhusiana na maisha yao (Brondsted, 2007). Utabiri huo ulikuwa sanjari na nguvu za miungu yenye dhima hiyo. Miungu hao walibashiri jinsi mtu atakavyozaliwa, mahali atakapozaliwa, namna atakavyoishi, jinsi atakavyokufa na sehemu atakapofia. Thomas (2011) anaongezea kuwa Wayunani wa kale walikuwa wanakwenda kwa waaguzi kwa lengo la kuuliza na kujulishwa kuhusu habari za jaala au kudra zao. Hata hivyo, kwa lolote waliloambiwa, ilikuwa vigumu kwa mtu kubadilisha yaliyopangwa na miungu anayohusiana nayo.

Kwa upande wa jamii za Waafrika, fikra za kijaala ziliegemezwa katika miungu ya mizimu. Murphy (2003) anadokeza kuwa Waafrika walikuwa na imani zao zilizoamini Mungu, miungu na mizimu. Miungu hiyo iliheshimiwa, kuthaminiwa na kuenziwa. Mungu aliutawala ulimwengu kupitia miungu na mizimu iliyokuwa ikiwajibika kwa mambo muhimu ya jamii kama vile uzazi, kilimo, mvua, kuponywa maradhi na kuondoa balaa. Mulokozi (1997) anatoa mfano kwa kutaja miungu mbalimbali walioaminiwa na kuabudiwa na watu wa jamii ya Wakiziba. Mungu wao mkuu ambaye ni muumbaji wa nchi na anga ni *Ruhanga*. Ruhanga alikuwa na miungu waliomsaidia ambao ni *Mugasha* (Mungu wa ziwa, upepo na mvua), *Lweru* (Mungu wa Ziwa Viktoria), *Nyakalembe* (Mungu wa kilimo), *Kasana* (Mungu wa uwindaji na ardhi), *Irungu* (Mungu wa mapori), *Lyang'ombe* (Mungu wa wafugaji), *Kaithura-Nkuba* (Mungu wa radi na dhoruba) na *Rugila* (Mungu wa uzazi).

Hivi sasa, imani ya ujaala imechukua mwelekeo mpya kwa baadhi ya watu Barani Afrika, hususani baada ya kuja kwa wageni kutoka Mashariki ya Kati (Waarabu) pamoja na Ulaya (Wazungu). Licha ya mambo yao mengine, wageni hao waliasisi na kueneza dini za kigeni (Uislamu na Ukristo) Barani Afrika. Kuja kwa dini hizi kumeubadili mtazamo huu wa ujaala kwa kuwaelekeza watu wake kuamini juu ya 'Mungu Mpya'. Tofauti hii ya kiimani miongoni mwa wanajamii kuhusiana na dhana ya ujaala, bado haiwatoi katika duara la kuamini kuhusiana na kani inayoongoza maisha yao. Wote huelekeza imani zao kuwa ipo kani yenye nguvu inayowaongoza binadamu, vyote vilivyomo pamoja na matukio yanayowakumba hapa ulimwenguni.

Imani kuhusu ujaala imekuwa ikiwawezesha wanajamii kuishi katika hali ya utu, uadilifu, hofu na kuridhika juu ya mambo yote yanayowakumba. Hali hii hutokana na jamii kuamini kuwa yote yanayotokea yanasababishwa na kani hiyo inayomtazama muda wote (Chacha, 1992). Katika ushairi wa Kiswahili, fikra za kijaala zinaonekana kujitokeza katika kazi za watunzi mbalimbali. Mlaga (2017) anasisitiza kuwa jambo hili litaendelea kuwepo maadamu watu wataendelea kuwa na imani juu ya kuwapo kwa Mungu. Makala hii imechunguza fikra za kijaala zinazosawiriwa katika ushairi wa Kiswahili.

## 2.0 Mbinu za Utafiti na Nadharia

Makala hii imechunguza fikra za kijaala zinazosawiriwa katika ushairi wa Kiswahili. Makala imetokana na utafiti wa kimaktaba. Data za msingi zilipatikana kutoka katika diwani teule za *Tungizi za Mnyagatwa* na *Diwani ya Midulu*. Njia ya usomaji na uchambuzi wa matini ilitumika kupata data zilizolengwa na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya usimbishaji wa maudhui. Matokeo yamewasilishwa na kujadiliwa kwa kutumia Nadharia ya Ujaala. Waasisi wa Ujaala kama mkabala wa kushughulikia sanaa ni wataalamu wa Kiyunani, Plato na Aristotle. Wananadharia hawa wanatazama jaala kama kani isiyoelezeka, nasibu na isiyo ya kibinafsi inayoamua matokeo ya matukio fulani (Wamitila, 2003). Pia, wanaamini kuwa kama jambo limepangwa kutendeka, haiwezekani kujaribu kuliepuka au kuliathiri kwa namna yoyote ile. Wanaongeza kuwa, matukio yote katika historia ya ulimwengu pamoja na visa vya maisha ya kila siku hukatiwa shauri na jaala au majaaliwa.

Nadharia hii inasisitiza kuwa maisha ya kila binadamu hayana budi kuufuata mkondo fulani ambao umepangwa na kani asiyoweza kuidhibiti. Mawazo ya wataalamu hawa yanatumulikia mihimili ya nadharia ya Ujaala. Mosi, vitu na mambo yote yaliyopo hapa duniani yamesanwa na Mungu. Pili, kila kiumbe ana fikra za kuwepo kwa kani asiyoweza kupambana nayo popote atakapokuwa. Tatu, juhudi za binadamu haziwezi kudhibiti wala kukwepa matukio yanayomtokea. Nne, maisha ya duniani ni nukta ndogo sana ya duara zima la maisha ya wanadamu. Mihimili hii tuliitumia katika ukusanyaji, uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa katika utafiti uliofanyika.

## 3.0 Fikra za Kijaala Zilizosawiriwa katika Diwani Teule

Mshairi wa diwani zilizotafitiwa amesawiri fikra za kijaala kwa kujiegemeza katika mambo matatu. Mambo hayo ni mianzo na miisho ya mashairi, falsafa

kuhusu uwezo wa kutunga mashairi na mielekeo ya vipengele mbalimbali vya maudhui.

### 3.1 Mianzo na Miisho ya Mashairi

Namna ya kuanza na kumaliza kazi ya kifasihi ni miongoni mwa masuala ya kifani. Washairi wa Kiswahili wamekuwa wakiomba dua na baraka kutoka kwa Mungu ili awape uwezo wa kufanikisha walichokiazimia kukiwasilisha. Pia, mwishoni mwa utungo humshukuru kwa kuwezeshwa kufanikisha. Vionjo wanavyotumia katika kuomba na kushukuru huko ni kutaja majina mbalimbali ya Mungu na kumsalia Mtume. Hali hii huonekana katika tenzi na mashairi ya watunzi wanaofuatilia dini zote, ingawa walio wengi ni wale wanaofuatilia dini ya Uislamu (Shariff, 1988 &Chacha, 1992).

Mshairi ambaye diwani zake zilitafitiwa amesawiri fikra za ujaala mwanzoni na mwishoni mwa baadhi ya mashairi yake. Mifano ya mashairi yaliyoanza kwa kusawiri fikra za kijaala. Mwandishi anaeleza:

> Bismillahi naanza, kwa jina lake Manani,
> Allahu ndiye wa kwanza, akhera na duniyani,
> Muumba mwenye kufunza, ya pepo na ya motoni,
> Kwake zetu shukurani.
> (Shairi la *Allah*, uk. 23).

> Wa kuanza kutajika, ni Allahu msifika,
> Katujaliya kufika, vitini twajikaliya,
> Wajibu wetu wa pili, kumuombea Rasuli,
> Yeye na zake ahali, rehema kuwafikiya.
> (Shairi la *Karibu Mgeni Wetu,* uk. 62).

Mifano hii michache inayakinisha hoja kuwa mshairi anasawiri fikra za kijaala mwanzoni mwa mashairi yake. Katika mifano hii, Mungu anatangulizwa kwa kusifiwa, kuombwa na kutajwa kwa majina kama vile Allahu, Muumba, Mola na Manani. Pia, mshairi anamwombea amani Rasuli (Mtume Muhammad). Mshairi amefanya hivi ili kuendeleza kaida maarufu ya kumtegemea Mungu katika utungaji wa kazi mbalimbali za ushairi wa Kiswahili. Kwa upande wa miisho, fikra za kijaala zimebainika katika mashairi ya *Umri Wazidi Kwenda* (Diwani ya *Tungizi za Mnyagatwa*) na *Juzi si Jana ni Leo* (Diwani ya *Diwani ya*

*Midulu*). Katika ubeti wa mwisho wa shairi la *Umri Wazidi Kwenda*, mshairi anasema:

> Nimefika kituoni, namshukru Swaburu,
> Kwani Sengo ana nini, nina Mwenyezi na nuru,
> Umri nauthamini, mmiliki ni Ghafuru,
> Nyinyi mwajifanya huru, hesabu zi Qiyamani (uk. 210).

Katika mifano hii, mshairi anamshukuru Mungu ambaye anamtaja kwa majina ya Swaburu (Mwenye subira), Mwenyezi (Mmiliki wa zama zote), Ghafuru (Mwenye kusamehe), Mola na Mpaji (Mwenye kutoa). Majina na mawazo haya yanaonesha namna mshairi anavyosawiri thamani ya kani ya Mungu katika maisha yake. Hizi ni fikra za kijaala.

### 3.2 Falsafa Kuhusu Uwezo wa Kutunga

Kiini cha falsafa hii ni kumuona mshairi kama mtu maalumu aliyeruzukiwa na Mungu kipaji cha kutunga mashairi. Ushairi huonwa kama sanaa yenye upekee ambayo inahitaji mtu mwenye kipawa ili aweze kuisana. Kwa hiyo, si kila mtu anaweza kuwa mshairi mzuri (Abedi, 1965 &Nassir, 1979). Mshairi wa diwani mbili zilizotafitiwa anaamini kuhusu Mungu kuwa chanzo cha uwezo wake wa kusana tungo za kishairi. Mshairi anashadadia hoja hii katika *Tungizi za Mnyagatwa*:

> Tungizi hizi kwa wema utakaoonekana umo, si wa mtu, si wa jamii bali ni nyunyizi, mawaga, chechezi za Uungu wake *Allah* (*s.w*) ampaye mtu tusomjuwa, ampaye kitu tusichokijuwa. Lionekalo la hovyo, mtunzi hakulikusudia kwani uwovu ni wa Iblis, na sina urafiki naye (uk. 241).

Maelezo hayo yanadhihirisha bayana fikra za kijaala. Mtunzi ana yakini moyoni mwake kuwa mashairi aliyoyatunga yana hadia kutoka kwa Mungu ambaye ameyanyunyuzia cheche za Uungu wake. Dondoo linatusisitizia kuwa kama kuna ovu litakaloonekana katika mashairi hayo, basi ni la ibilisi ambaye mtunzi hana urafiki naye.

### 3.3 Mielekeo ya Maudhui ya Mashairi Yake

Mshairi amewasilisha mawazo mbalimbali yenye mwelekeo wa kusawiri ujaala katika diwani zake mbili zilizotafitiwa. Makala hii imeyasinyaza mawazo hayo katika makundi mbalimbali. Baadhi yake ni uhai, ndoa, uzazi, maradhi na kifo.

### 3.3.1 Uhai

Uhai ni hali inayomwezesha kiumbe kuishi duniani. Uhai ni kinyume cha ufu. Wanaujaala wanaamini kuwa uhai huanzishwa, hudhibitiwa na kutamatishwa na Mungu. Kila kiumbe huwa na muda maalumu wa kuishi hapa duniani (Hassan, 2018). Katika jitihada za kuthamini uhai na kuona kuwa ni hidaya ambayo mja amekirimiwa na Mungu, watu wamekuwa wakimshukuru Mungu muda wote kwa kuwajaalia kuendelea kupumua mpaka muda huo. Mshairi wa diwani teule ameuzungumzia uhai kwa kutumia fikra za kijaala. Katika diwani ya *Tungizi za Mnyagatwa*, kuna shairi la *Allah* linalosawiri fikra za kijaala. Katika ubeti wa tatu, mshairi anasema:

> Nasi tuzidi ibada, ndugu zangu sikizeni,
> Uhai si wa kubweda, ni mwingi wa mitihani,
> Kina kaka kina dada, tuwache ya ujanani,
> Kwa *Allah* ndiko rejeyo (uk. 218).

Mshairi anaikumbusha jamii kutojisahau na uhai walionao kwa sababu ni mali ya Mungu. Anaikumbusha zaidi kwamba kila chenye mwanzo kina mwisho. Hivyo, watu wautumie uhai wao vizuri kwa kumcha Mungu ambaye kila kiumbe hapa duniani kitarejea kwake. Fikra hii inaumana vyema na mhimili wa Nadharia ya Ujaala kuwa maisha ya duniani ni nukta ndogo sana ya duara la maisha ya wanadamu.

Pia, katika shairi la *Al-Hamdu-Lillah!*, mshairi anamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumjaalia uhai na afya njema. Pia, anaikumbusha jamii kuhusu kumcha Mungu pamoja na wazazi wawili, baba na mama. Ubeti wa sita wa shairi hili unaizindusha jamii kuhusiana na suala la kuumbwa kwao, uhai walionao, pamoja na yote wanayotendewa na Mungu hapa ulimwenguni. Mshairi anasema:

> Uumbizi na uhai, uzima pamwe huduma,
> Ni zaidi ya jinai, tukisahau ya nyuma,
> Bora kujirairai, dini si ya nyumanyuma,
> Wa pili baba na mama, *Ali-hamdulillah*! (Uk. 226).

Katika ubeti huu, mshairi anausawiri uhai kwa kuuegemeza katika fikra za kijaala kuwa Mungu ndiye mwenye mamlaka nao. Mshairi anaiambia jamii kuwa ni kosa la jinai kusahau namna ya kuumbwa kwao, aliyewaumba, uhai

wao pamoja na huduma zote wanazotendewa na aliyewaumba (Mungu). Hivyo, anaitaka jamii kujibiidisha katika kuishika dini.

### 3.3.2 Ndoa

Ndoa ni mkataba wa hiyari baina ya mwanamke na mwanamume kuishi pamoja kama mume na mke. Kuoa au kuolewa ni jambo la lazima kwa mtu aliyefikia umri unaokubalika na jamiii husika. Ulazima huo unatokana na haja za maumbile ya mtu binafsi pamoja na haja za mazingira ya ulimwengu unaomzunguka (Sengo, 2008). Kila jamii ina taratibu zake za kuiendea ndoa. Zipo jamii zinazojigeza katika misingi ya dini za kijadi kwa kufanya ibada maalumu ya kuwaombea maharusi kabla na baada ya ndoa.

Pia, zipo jamii zinazozingatia mafundisho yaliyomo kwenye vitabu vitakatifu vya dini za Ukristo na Uislamu, yaani Biblia na Kurani mtawalia (Hassan, 2018). Makala hii inalinasibisha suala la ndoa na fikra za kijaala kutokana na imani waliyonayo wanajamii kuwa 'Ndoa hupangwa mbinguni', yaani, hupangwa na Mungu. Kila mmoja anapoingia katika umri wa kuoa au kuolewa huomba Mungu amjaalie mke au mume bora wa kudumu naye maishani. Katika diwani ya *Tungizi za Mnyagatwa*, kuna shairi la *Mirathi* linalohusianisha suala la ndoa na kani ya Mungu. Mshairi anasema:

> Nikazipiga sigida, nyingi za kuomba mke,
> Dua nyingi nizigida, kupata aso makeke,
> Nikampata Seyyida, yatima mpwekepweke (uk. 49).

Katika ubeti huu, mshairi anadhihirisha imani yake kuwa alikithirisha sala na dua kwa Mungu ili ampatie mke mwema na, hatimaye, dua lake likakubaliwa na Mola kwa kumpata mke mwema. Pia, katika diwani hiyohiyo kuna shairi la *Wake Zangu* linalodhihirisha fikra za kijaala kuhusiana na ndoa. Mshairi akimshukuru Mungu kwa kumjaalia kuoa, anatongoa hivi:

> Namshukuru Manani, kunijaliya kuowa,
> Fatuma wa Udigoni, Songeya alikozawa,
> Tukutana Mngotini, ambako alilelewa,
> Si tajiri masikini, kwa hali alivyokuwa,
> Ndiye wa kwanza nyumbani (uk.102).

Mifano hiyo inaonesha jinsi ndoa inavyohusishwa na mawazo ya kijaala. Watu wamekuwa wakimuomba Mungu awajaalie kupata wenza wema ambao wataungana nao katika kuyajenga maisha. Kitendo hiki cha mwanadamu kumuelekea Mungu katika mambo yake kinadhihirisha wazi kuwa matendo, nia na mustakabali wa maisha yake hapa ulimwenguni yanaamuliwa na jaala.

### 3.3.3 Uzazi

Uzazi ni jambo ambalo binadamu hatuna uwezo nalo. Katika jamii ya Waswahili, uzazi huchukuliwa kuwa jambo la majaaliwa ambalo linaidhinishwa na Mungu (Sengo, 2008). Jambo hili linadhihirika pia kupitia semi za Kiswahili kama vile kuolewa ni sheria, kuzaa majaaliwa. Msingi mmojawapo wa ujaala unatuelekeza kuwa vitu na mambo yote yaliyoko hapa duniani yameumbwa na Mungu. Miongoni mwa mambo hayo ni uzazi. Inapotokea kuwa wanandoa wamekaa muda mrefu bila kujaaliwa watoto, jitihada mbalimbali hufanywa ili kumuomba Mungu. Maombi hayo hufanywa kulingana na itikadi ya wanandoa husika pamoja na ndugu au/na jamaa. Hivyo, huweza kufanywa kwa kuzingatia miongozo ya kijadi, Kikristo au Kiislamu. Shairi la *Ithineni Majaliwa* lililomo katika *Diwani ya Midulu* linaonesha imani ya mshairi katika suala zima la uzazi. Mshairi anasema:

> Namshukuru Wahabu, kunijaliya thineni,
> Wote kwangu mahabubu, ni tunu mwangu moyoni,
> Kwa ndowa za taratibu, kwa radhi yako Manani,
> Sikujuwa sikudhani, baba mmoja kwa babu (uk. 20).

Katika ubeti huu, tunamuona mshairi akimshukuru Mungu kwa kumjaalia watoto wawili ambao wamepatikana baada ya kuishi kwa muda mrefu na mkewe wa awali bila kupata mtoto. Mtunzi anaonesha kuwa mwenye uwezo wa hilo ni Mungu. Anabainisha zaidi jambo hili katika ubeti wa tatu. Anasema:

> Ishirini ilipita, miyaka mke Fatuma,
> Bahati hatukupata, kushika hakukufuma,
> Kumbe mambo yamkuta, mahaba ya wake mama,
> Si kazi kurudi nyuma, kupata kuna utata.

Baada ya miaka 20 ya kuishi bila kupata mtoto kutoka kwa mkewe wa awali, Bi. Fatuma, mshairi aliwaoa wake wengine wawili, Bi. Zawadi na Bi. Jamillah. Hawa walimpatia watoto wawili, Yusufali na Khalifah. Mshairi anaonesha

imani yake kuwa uzazi hutoka kwa Mungu anapotuambia kuwa kupatiwa watoto wawili siyo makusudi yake, bali ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Pia, anazidi kuomba dua ili apate watoto zaidi kwa mkewe wa nne, Bi. Sheikha. Ushikamani wa fikra hii unapata nguvu tunaposoma shairi la *Mirathi* (uk. 49) katika diwani ya *Tungizi za Mnyagatwa*. Shairi hilo linaeleza kuhusiana na Mwenyezi Mungu alivyoutibu utasa kwa Bi. Jamilah na hatimaye, akamjaza heri kwa kushika ujauzito na kuzaliwa Khalifah. Mshairi anaandika:

> Kasilimu kwa khiyari, kabla ndowa kujibu,
> Allah kamjaza kheri, utasa akautibu,
> Kazaliwa mshauri, Khalifah wetu muhibu.

Mifano hiyo inakazia ukweli wa jinsi dhana ya uzazi inavyofungamanishwa na ujaala. Hali hii ni kwa sababu mwanadamu huamini kuwa mambo yote yameshapangwa na Mungu, hivyo hana budi kuyapokea.

### 3.3.4 Maradhi

Maradhi ni kitu kinachompata mtu au mnyama na kuathiri afya yake. Fikra za kijaala huhusisha maradhi na Mungu; kwamba, ndiye humpa maradhi mja amtakaye na kumponya amtakaye. Wafuasi wa ujaala wa kijadi huhuhusisha maradhi na Miungu na mizimu; ndiyo maana, mtu anapougua hupelekwa kwa mizimu au waganga ili kuendesha mchakato wa uponyaji. Wafuasi wa ujaala wa kisasa huitakidi kuwa maradhi hushushwa na Mungu. Wafuasi hawa hufuata tiba za hospitalini pamoja na maombezi kutoka kwa wabobezi wa dini ambao hufanya kwa kutumia miongozo ya vitabu vitakatifu. Katika *Diwani ya Midulu*, mshairi anaonesha fikra zake kuhusu fikra za kijaala kuhusiana na maradhi kupitia shairi la *Bwana Mwarabu Saidi.* Anasema:

> Tangu upate maradhi, bwana Mwarabu Saidi,
> Sijapata kukukidhi, kwa kitu cha ushahidi,
> Ila duwa za hifadhi, na pilika za ahadi,
> Bwana Mwarabu Saidi,
> Pole sana kwa maradhi.
>
> Tiba nikakufanyiya, na safari kujituma,
> Leo tutakusomeya, duwa yenye kuzizima,
> Allah ataipokeya, maradhi atayazima,
> Bwana Mwarabu Saidi,

Pole sana kwa maradhi (uk. 81).

Katika beti hizi mbili, tunamuona mshairi akiamini kuwa maradhi huondoshwa na Mungu kupitia dua. Fikra hizi zinadhihirika pia katika *Tungizi za Mnyagatwa*, kupitia shairi la *Uganga*. Ubeti wa pili una mishororo ifuatayo:

Aliyeumba maradhi, ndiye mwenye lahaula,
Kila tiba ina radhi, Allah hupokeya sala,
Halikidhi halikidhi, hata la kinyamkela,
Ila kwa yake hifadhi, na kubuli zake Mola,
Uganga! (uk. 7).

Mshairi anayakinisha kuwa maradhi yameumbwa na Mungu. Mungu ndiye mponyaji wa maradhi yote kwa kadri atakavyo. Pia, anawashajiisha watu kumwomba Mungu kwa sababu mgonjwa hupona baada ya dua yake kukubaliwa.

**3.3.5 Kifo**

Kifo ni hali ya kiumbe kufikia mwisho wa uhai. Wafuasi wa ujaala wa kijadi huamini kuwa wafu huwa bado wana uhai. Aidha, huamini kuwa watu hawafi bali hujificha. Pia, wanaamini kwamba wafu na walio hai huendelea kuwa na uhusiano wa karibu (Sengo, 1995). Mtazamo wa wafuasi wa ujaala wa kisasa (Ukristo na Uislamu) unahusisha dhana ya kifo na nguvu au mipango ya Mungu. *Biblia Takatifu* inabainisha suala hili katika kitabu cha *Mwanzo*, 3:19 kuwa: ‘Kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi’ (Chama cha Biblia cha Tanzania, 1997).

Pia, Kurani inalizungumzia suala hili katika sura mbalimbali. Sura ya 3:186 inabainisha: “Kila nafsi itaonja umauti, na bila shaka mtapewa ujira wenu sawasawa siku ya kiyama. Aliyewekwa mbali na moto na kuingizwa peponi, basi amefaulu na maisha ya dunia hii si kitu ila ni starehe idanganyayo”. Sura ya 21:36 inaeleza: “Kila nafsi itaonja umauti na tutakujaribuni kwa shari na heri, na kwetu mtarejeshwa” (Al-Farsy, 1969).

Kutokea kwa kifo huchukuliwa kuwa ni kutimia kwa maandiko ya Mungu kwa mja wake. Hii ndiyo sababu ya kuwapo kwa kauli kama vile “Kazi ya Mungu,

haina makosa". Sengo (2008) anaeleza kuwa watu wenye imani kuhusu uwezo wa Mwenyezi Mungu huyatazama maisha kama safari fupi, nzuri na ya haraka. Mtu hupewa nafasi hiyo ya kusafiri ili aweze kuona sehemu tu za mifano ya kila namna kuhusu maisha ya kweli na ya kudumu. Anaongeza kuwa, maisha yote yamejaa majaribu ya namna mbalimbali na, kwamba, maisha si yake.

Matapo yote haya mawili ya ujaala wa kisasa yanaamini kuhusu kuwapo kwa maisha baada ya kufa; ambapo roho ya mfu huhifadhiwa mahali fulani milele na milele. Pia, huamini kuhusu kufufuliwa na kupewa malipo yanayotokana na matendo ya mtu akiwa duniani. Mtu aliyeishi kwa kufuata maamrisho ya Mungu huingizwa peponi na yule muovu huingizwa motoni. Kwa hiyo, kifo kinapotokea, waumini wa kundi hili hufanya jitihada za kumwomba Mungu ili ampokee maiti wao pamoja na kumpa makazi mema huko aendako. Katika diwani ya *Tungizi za Mnyagatwa*, kuna shairi la *Twakutakiya Rehema Dida Wetu Kibokoni* linaeleza fikra hii ya kifo na kuihusisha na ujaala. Mshairi anasema:

> Ni Mola ndiye mneni, mwenye kumiliki "Kuni,"
> Kila roho qiyamani, tapitiya kaburini,
> Kwetu sote mtihani, imesema Quruwani,
> Dida sasa yu mavani, na sisi tuko nyumbani.
> Nyumbani roho kutokwa, si khiyari ni lazima,
> Nafsi ni kama kokwa, mmeya kihimahima,
> Uhai wetu kupokwa, katupangiya Rahima,
> Twamtakiya rehema, Dida wetu Kibokoni (uk. 94).

Mshairi anaamini kuwa kifo ni kazi ya Mungu na mauti ni mlango ambao kila kiumbe atapitia. Kwa kuwa fikra za ujaala huu huamini kuwa anayekufa hurudi kwa Muumba wake, wanaobaki huzidi kumuombea dua ili maiti apumzishwe mahali pema kama mshairi anaposema, 'Twamtakiya rehema, Dida wetu Kibokoni'. Katika *Diwani ya Midulu* kuna shairi la *Ramadhani wa Hassani*linalooonesha kuwa fikra ya kifo inafungamana na ujaala. Pia, linabainisha kuwa kifo hupangwa na Mungu na wajibu wa wanaobaki ni kumuombea dua njema maiti wao. Mshairi anasema:

> Umetuwaga mwenetu, Ramadhani wa Hassani,
> Sungu da udele jetu, umefika kaburini,
> Ahadi ya Mola wetu, asiye na mshindani,

Yapozwe yalo mavani, ukapumuwe mwakwetu.

Duwa tunakuombeya, upokelewe peponi,
Mungu atakupokeya, akuweke pa amani,
Adhabu kukufutiya, akutowe madhambini,
Nasi tumo msibani, hatwishi kukuliliya (uk. 49).

Dhana ya kifo, kama fikra mojawapo ya kijaala, inatilia nguvu imani ya wanaujaala kuwa mwanadamu hawezi kuyakwepa matukio aliyopangiwa na Mungu. Matukio mengine kama vile uzee, ajali na maradhi huchukuliwa kama viambata tu vinavyowezesha tukio hilo kubwa la kijaala kutokea. Ndiyo maana, ijapokuwa mwanadamu hujitahidi katika kujinasua na kifo, mathalani kwa mgonjwa kwenda au kupelekwa hospitali kwa lengo la kupatiwa tiba, lakini Mungu hupitisha kani yake kwa kumtwaa kiumbe wake.

**4.0 Hitimisho**

Makala hii imebainisha namna fikra za ujaala zinavyosawiriwa katika ushairi wa Kiswahili. Mjadala ulijiegemeza kwenye diwani mbili za *Tungizi za Mnyagatwa* na *Diwani ya Midulu*. Msanii amesawiri ujaala kupitia mambo matatu. Jambo la kwanza ni mianzo na miisho ya mashairi. Mtunzi ameanza na kumaliza baadhi ya mashairi yake kwa kumtaja, kumsifu, kumshukuru na kumwomba Mungu. Jambo la pili ni falsafa kuhusu uwezo wa kutunga mashairi. Diwani zilizotafitiwa zimeonesha kuunga mkono fikra inayoaminiwa na watunzi wengi wa mashairi kuwa ushairi ni sanaa inayohitaji karama maalumu kutoka kwa Mungu.

Jambo la tatu ni mielekeo ya vipengele mbalimbali vya maudhui. Mtunzi amesawiri fikra za kijaala kupitia vipengele mbalimbali. Baadhi yake ni uhai, ndoa, uzazi, maradhi na kifo. Kwa kuwa diwani zilizotumika ni za mshairi anayetokea katika jamii ya Waislamu, ni wazi kuwa kijitapo cha ujaala kilichochukua nafasi kubwa katika makala hii ni ujaala wa Kiislamu. Makala hii inapendekeza tafiti zaidi zifanyike kuhusu mdhihiriko wa ujaala wa matapo mengine katika tanzu mbalimbali za fasihi, uwezo na kiasi cha tanzu nyingine za fasihi ya Kiswahili kusawiri ujaala, kulinganisha uwezo na kiasi cha usawiri wa ujaala kati ya fasihi na tawi lingine lolote la sanaa na kulinganisha mdhihiriko wa ujaala katika fasihi ya jamii ya Waswahili na ya jamii ya nje ya Waswahili.

**Marejeleo**

Abedi, K. A. (1965). 'Utangulizi' katika Mnyampala, M. *Waadhi wa Ushairi*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Al-Farsy, A. S. (1969). *Tafsiri ya Qurani Tukufu*. Nairobi: The Islamic Foundation.

BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.

Brondsted, M. (2007). *The Transformations of the Concept of Fate in Literature*. Oxford: Oxford University Press.

Chacha, C. N. (1992). *Ushairi wa Abdilatif Abdalla*: *Sauti ya Utetezi*. Dar es Salaam: Dar esSalaam University Press.

Chama cha Biblia cha Tanzania, (1997). *Biblia: Maandiko Matakatifu*. Dodoma: The BibleSociety of Tanzania.

Chuachua, R. (2016). *Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katikaMuktadha wa Epistemolojia ya Kibantu*. Tasinifuya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Cicero, M. T. (1962). *On Old Age*. (Mh na mf. Andrew Preston). Cambridge: CambridgeUniversity Press.

Cuddon, J. A. (1998). *The Penguin Dictionary of Literary Terms and Literary Theory 4th Edition*. London: Penguin Books.

Hameed, S. (2011). Is Islam a Religion of Fatalism? Ilisomwa Aprili 11, 2022 katika http://www.irfi.org/articles/articles.htm.

Hassan, H. R. (2018). Ujaala katika Ushairi wa Kiswahili: Mifano Kutoka *Tungizi zaMnyagatwa* na *Diwani ya Midulu*. Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mlaga, W. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.

Mulokozi, M. M. (1997). *Utenzi wa Nyakiiru Kibi*. Morogoro: Ecol Publications.

Murphy, G. L. (2003). *African - American Faith in America*. Oxford: Oxford University Press.

Nassir, A. (1979). 'Dibaji' katika *Utenzi wa Mtu ni Utu*. London: Macmillan Education Ltd.

Nkwera, F. M. V. (1976). "Fasihi" katika *Uandishi wa Tanzania* (Mh. J. M. Mbonde). Nairobi: East African Literature Bureau.

Origen, A. (1960). *On First Principal*. (Mh., na mf., A. O. Robert). London: George Fox University Press.

Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.

Ponera, A. S. (2010). Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert: Maana Yake, Sababu za Kutumiwa na Athari Zake kwa Wasomaji.Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Sengo, T. S. Y. (2010). *Diwani ya Midulu*. Dar es Salaam: Al-Amin Education and Research Academy.

Sengo, T. S. Y. (2009). *Tungizi za Mnyagatwa*. Dar es Salaam: Al-Amin Education and Research Academy.

Sengo, T. S. Y. (2008). *Tafakuri ya Utu na Uhai*. Dar es Salaam: Huda Publishers.

Sengo, T. S. Y. (1995). "Itikadi katika Jamii za Kiswahili" katika *Lugha, Utamaduni na FasihiSimulizi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Senkoro, F. E. M. K. (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity City.

Shariff, I. N. (1988). *Tungo Zetu*. Trenton: The Red Sea Press Inc.

Thomas, R. (2011). "Taswira ya Nyoka katika Ngano za Kiswahili: Mifano Kutoka Milima ya Usambara". Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi*: *Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.